MAWASILISHO YA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2018/19

Mawasilisho ya Mpango na Bajeti ya Fungu 78: Mkoa wa Mbeya kwa mwaka 2018/19 yanahusisha; Makadirio ya makusanyo ya Mapato ya Ndani (Own sources), Ruzuku kutoka Serikali Kuu pamoja na Wadau wa Maendeleo. Fedha hizi zinatarajiwa kutumika kulipa Mishahara ya watumishi, kugharamia Matumizi Mengineyo pamoja na kugharamia Miradi ya Maendeleo. Aidha, Bajeti ya Mishahara iliyotengwa itatumika kulipa Watumishi waliopo katika Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Mkoa wa Mbeya.

VIPAUMBELE VILIVYOZINGATIWA KATIKA KUANDAA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2018/19

Mpango na Bajeti ya Fungu 78 Mkoa wa Mbeya pamoja na Halmashauri zake kwa mwaka 2018/19 umeandaliwa kwa kuzingatia Vipaumbele vifuatayo:

i. Kuongeza ukusanyaji wa Mapato ya Ndani (Own Sources) ili kuwezesha Halmashauri kutoa huduma kwa wakati na kwa ufanisi
ii. Kuboresha miundombinu itakayochochea maendeleo ya sekta za Uchumi.
iii. Kutoa huduma za Ugani kwa lengo la kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo.
iv. Kuboresha utoaji wa huduma za kijamii (Elimu, Afya na Maji) ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vyoo, madarasa, nyumba za walimu, ujenzi wa zahanati na vituo vya afya pamoja na kuongeza mtandao wa upatikanaji wa maji safi na salama.
v. Kutenga fedha kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika mwaka 2019
vi. Kutenga fedha kwa ajili ya kuviwezesha Vikundi vya Wanawake na Vijana

MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA 2018/19

Makadirio ya Mapato kwa mwaka 2018/19 kwa Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri kwa maeneo yasiyo ya ruzuku (own source) ni kama ilivyo katika Jedwali Na.1.

Jedwali Na. 1: Makadirio ya Mapato ya Mkoa kwa Mwaka 2018/19

S/N	Taasisi	Makadirio ya Mapato mwaka 2018/19	kwa Ajili ya Miradi ya Maendeleo	kwa Ajili ya Matumizi ya Kawaida
1	2	3	4	6
1	RS	5,543,000	0	0
2	Mbeya CC	12,942,473,000	5,646,123,000	7,296,350,000
3	Chunya DC	2,850,722,000	1,127,043,000	1,723,679,000
4	Kyela DC	3,918,149,000	1,570,424,000	2,347,725,000
5	Rungwe DC	4,485,423,000	1,881,367,000	2,604,056,000
6	Mbeya DC	2,958,119,000	1,553,342,000	1,404,777,000
7	Mbarali DC	4,711,352,000	1,839,249,000	2,872,103,000
8	Busokelo DC	756,300,000	169,466,000	586,834,000
Jumla - LGAs		**32,622,538,000**	**13,787,014,000**	**18,835,524,000**
TOTAL - MKOA		**32,628,081,000**	**13,787,014,000**	**18,835,524,000**

Halmashauri za Wilaya na Jiji zimetenga jumla ya **Sh. 2,437,692,609** kwa ajili ya Mfuko wa Wanawake na Vijana. Kati ya fedha hizo **Sh. 1,218,846,304** kwa ajili ya Mfuko wa Wanawake na **Sh. 1,218,846,304** kwa ajili ya Mfuko wa Vijana. Fedha hizi zimelenga kukopesha vikundi mbalimbali vya wanawake na vijana ili kuendeleza jitihada za kujikwamua kiuchumi. Jedwali Na. 2 linaonesha mchanganuo wa fedha zilizotengwa.

Jedwali Na. 2; Fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mfuko wa Wanawake na Vijana kwa mwaka 2018/19

NA.	HALMASHAURI	Mfuko wa Wanawake (5%)	Mfuko wa Vijana (5%)	JUMLA
1	Chunya DC	132,876,143	132,876,143	**265,752,286**
2	Busokelo DC	37,815,000	37,815,000	**75,630,000**
3	Rungwe DC	185,050,500	185,050,500	**370,101,000**
4	Mbeya DC	147,905,960	147,905,960	**295,811,920**
5	Mbeya CC	475,182,650	475,182,650	**950,365,300**
6	Mbarali DC	164,275,000	164,275,000	**328,550,000**
7	Kyela DC	75,741,051	75,741,051	**151,482,102**
	JUMLA	**1,218,846,304**	**1,218,846,304**	**2,437,692,608**

MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA 2018/19

Katika mwaka wa fedha 2018/19 Mkoa umekadiria kutumia **Sh. 224,863,082,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Mishahara (PE) ni **Sh. 195,522,403,000.00** na Matumizi Mengineyo (OC) ni **Sh. 29,340,679,000.00.**

SEKRETARIATI YA MKOA

Jumla ya **Sh. 7,921,636,000.00** zimetengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Sekretariati ya Mkoa. Kati ya fedha hizo, **Sh. 6,358,551,000.00** ni Mishahara na **Sh. 1,563,085,000.00** ni Matumizi Mengineyo kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 3 hapa chini.

Jedwali Na. 3: Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida ya Sekretarieti ya Mkoa

Kifungu	Jina la Kifungu	Mshahara	Matumizi Mengineyo	Jumla
1001	Utawala na Usimamizi wa Watumishi	816,836,000	482,750,000	1,299,586,000
1002	Fedha na Uhasibu	132,831,000	20,000,000	152,831,000
1003	Ukaguzi wa Ndani	50,088,000	10,000,000	60,088,000
1004	Usimamizi wa Manunuzi	69,381,000	8,000,000	77,381,000
1005	DAS Mbeya	224,510,000	81,155,000	305,665,000
1007	DAS Kyela	178,386,000	80,461,000	258,847,000
1008	DAS Chunya	148,090,000	80,509,000	228,599,000
1010	DAS Rungwe	190,222,000	80,700,000	270,922,000
1011	DAS Mbarali	153,510,000	79,863,000	233,373,000
1014	Huduma za Sheria	25,764,000	8,000,000	33,764,000
1015	Kitengo cha TEHAMA	39,180,000	12,000,000	51,180,000
2001	Mipango na Uratibu	93,882,000	60,000,000	153,882,000
2002	Uchumi na Uzalishaji	192,336,000	50,000,000	242,336,000
2003	Miundombinu	197,778,000	50,000,000	247,778,000
2004	Huduma za Jamii	0	25,000,000	25,000,000
2005	Usimamizi wa Serikali za Mitaa	125,508,000	30,000,000	155,508,000
2006	Sekta ya Elimu	105,396,000	394,647,000	500,043,000
2007	Sekta ya Maji	74,121,000	10,000,000	84,121,000
3001	Regional Hospital	3,540,732,000	0	3,540,732,000
JUMLA		**6,358,551,000**	**1,563,085,000**	**7,921,636,000**

SERIKALI ZA MITAA

Katika Mwaka 2018/19 Bajeti za Matumizi ya Kawaida kwa Serikali za Mitaa zinajumuisha Ruzuku kutoka Serikali Kuu na Fedha zinazokusanywa kutokana na vyanzo vya Ndani (own sources).

Katika mwaka 2018/19 Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekadiria kutumia jumla ya **Sh. 216,941,446,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo Mishahara ni **Sh. 189,163,852,000.00 na** Matumizi Mengineyo ni **Sh. 27,777,594,000.00** Mchanganuo wa Makadirio ya matumizi ya Kawaida ya Halmashauri umeoneshwa katika jedwali Na. 4.

Jedwali Na. 4: Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa kila Halmashauri

Halmashauri	Mishahara	Matumizi ya Mengineyo	Jumla
Mbeya CC	42,631,172,000	8,994,189,000	51,625,361,000
Chunya DC	15,005,540,000	2,678,773,000	17,684,313,000
Kyela DC	23,333,268,000	3,531,221,000	26,864,489,000
Mbeya DC	31,661,333,000	3,105,985,000	34,767,318,000
Rungwe DC	36,445,182,000	4,075,851,000	40,521,033,000
Mbarali DC	27,358,758,000	4,016,333,000	31,375,091,000
Busokelo DC	12,728,599,000	1,375,242,000	14,103,841,000
JUMLA	**189,163,852,000**	**27,777,594,000**	**216,941,446,000**

MAKADIRIO YA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2018/19

Katika Mwaka 2018/19, Mkoa umekadiria kutumia jumla ya **Sh. 55,832,670,500** kwa ajili ya kutekeleza Programu na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Sh. 35,276,662,500** ni Fedha za Ndani na **Sh. 20,556,008,000** ni Fedha za Nje.

SEKRETARIETI YA MKOA:

Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Sekretarieti ya Mkoa ni kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 5.

Jedwali Na.5: Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo ya Sekretarieti ya Mkoa

NAMBA YA MRADI	JINA LA MRADI	FEDHA YA NDANI	FEDHA YA NJE	JUMLA
6532	Mfuko wa Kujitegemea (RC na DCs)	45,000,000	-	45,000,000
6318	Ukarabati wa Ofisi za Serikali – Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya na Ofisi za Wakuu wa Wilaya ya Chunya, Mbarali na Kyela	168,895,000	-	168,895,000
6339	Ukarabati wa Nyumba za Serikali – Nyumba ya Mkuu wa Mkoa, Nyumba ya Katibu Tawala wa Mkoa, Nyumba za Wakuu wa Wilaya za Mbarali, Rungwe, Chunya na Mbeya; na Nyumba za Makatibu Tawala wa Wilaya za Kyela, Rungwe, Mbarali, Chunya na Mbeya	701,400,000	-	701,400,000
3280	Programu ya usambazaji maji na usafi wa mazingira vijijini (RWSSP)	-	66,774,000	66,774,000
6389	Ujenzi wa Ofisi za Serikali – Ofisi za Maafisa Tarafa za Kiwanja (Chunya), Ikukwa (Rungwe) na; Isangati na Tembela (Mbeya)	360,000,000	-	360,000,000
6517	Msaada wa UNICEF katika Kuimarisha Usimamizi na Ufuatiliaji Kisekta	-	437,605,000	437,605,000
4390	Programu ya Kuendeleza Elimu ya Sekondari (SEDP)	24,463,000	-	24,463,000
6251	Mradi wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma	-	160,000,000	160,000,000
6531	Kufuatilia na Kutathmini	535,000,000	-	535,000,000

NAMBA YA MRADI	JINA LA MRADI	FEDHA YA NDANI	FEDHA YA NJE	JUMLA
	Utekelezaji wa Programu za Umma			
4486	Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo [ASDP)	13,242,000	-	13,242,000
4553	Mfuko wa Uendelezaji Zao la Ngozi	2,000,000	-	2,000,000
5421	Programu ya Kuboresha Afya (HSBF)	-	126,094,000	126,094,000
	JUMLA	**1,850,000,000**	**790,473,000**	**2,640,473,000**

HALMASHAURI

Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Halmashauri ni kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 6.

Jedwali Na. 6: Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Halmashauri

NAMBA YA MRADI	JINA LA MRADI	FEDHA YA NDANI	FEDHA YA NJE	JUMLA
3280	Programu ya usambazaji maji vijijini na usafi wa mazingira (RWSSP)	-	3,730,904,000	3,730,904,000
4322	Programu ya Uendelezaji wa Elimu ya Msingi Bure	4,918,950,000	-	4,918,950,000
4393	Programu ya Uendelezaji wa Elimu ya Sekondari Bure	7,539,737,500	-	7,539,737,500
4946	Miradi ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri (Own Source Projects)	13,787,014,000	-	13,787,014,000
6209	Mfuko wa Jimbo	380,961,000	-	380,961,000
5421	Mpango wa Pamoja wa Kuboresha Afya (HSBF)		3,306,237,000	3,306,237,000
6401	Miradi ya Halmashauri ya Wilaya	2,300,000,000	-	2,300,000,000
6403	Programu ya kuendeleza Jiji la Mbeya (TSCP)	-	8,960,235,000	8,960,235,000
6517	Msaada wa UNICEF katika Kuimarisha Usimamizi na Ufuatiliaji Kisekta	-	3,768,159,000	3,768,159,000
6205	Ujenzi wa Hospitali za Wilaya	4,500,000,000	-	4,500,000,000
Jumla		**33,426,662,500**	**19,765,535,000**	**53,192,197,500**